TANGAZO LA SERIKALI NA. 164 la tarehe 15/3/2024

SHERIA YA HAKIMILIKI NA HAKISHIRIKI,
(SURA YA. 218)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 54G)*

KANUNI ZA MAREKEBISHO YA KANUNI ZA HAKIMILIKI NA HAKISHIRIKI (KAMPUNI ZA KUKUSANYA NA KUGAWA MIRABAHA), 2024

Jina
TS Na. 215 la 2023

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Marekebisho ya Kanuni za Hakimiliki na Hakishiriki (Kampuni za Kukusanya na Kugawa Mirabaha) za Mwaka 2024 na zitasomwa pamoja na Kanuni za Hakimiliki na Hakishiriki (Kampuni za Kukusanya na Kugawa Mirabaha) za Mwaka 2023 ambazo zitarejewa humu kama "Kanuni kuu".

Marekebisho ya kanuni ya 3

2. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 3 kwa kufuta kanuni ndogo ya (2) na badala yake kuweka kuweka kanuni ndogo ifuatayo-

"(2) Kwa kuzingatia masharti yaliyotajwa katika kifungu cha 52C cha Sheria, kampuni haitaweza kuomba leseni isipokuwa kama Bodi na menejimenti ya kampuni itaundwa na raia wa Tanzania na kimsingi wawe wanaishi Tanzania.

Marekebisho ya kanuni ya 16

3. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 16 kwa kufuta kanuni ndogo ya (4).

Marekebisho ya kanuni ya 27

4. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 27 kwa-

(a) kufuta kanuni ndogo ya (3) na badala yake kuweka kanuni ndogo zifuatazo-

"(3) Endapo Ofisi imeridhika kwamba kampuni ya kukusanya na kugawa mirabaha inakiuka masharti ya kanuni ndogo ya (1) au (2), Ofisi itaitaarifu kampuni hiyo kuwasilisha utetezi kuhusu ukiukwaji ndani ya siku thelathini tangu kupokea kwa taarifa.

(4) Endapo, kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (3) itathibitika kwa Ofisi kuwa-

(a) kampuni ya kukusanya na kugawa mirabaha inakiuka masharti ya kanuni ndogo ya (1) au (2) bila sababu za msingi; au

(b) kampuni ya kukusanya na kugawa mirabaha imeshindwa bila sababu za msingi kuwasilisha maelezo katika muda uliopangwa,

kampuni na maafisa wake watastahili kupata onyo la maandishi na kutakiwa kurekebisha ukiukaji huo ndani ya muda utakaotajwa."; na

(b) kubadili mpangilio wa kanuni ndogo ya (4) kuwa kanuni ndogo ya (5).

Dodoma,
28 February, 2024

PINDI H. CHANA,
*Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo*